



صبح بہاراں



# Upambazuko Wa Asubuhi

(Swahili)

Sheikh-e-Tariqat, Amir-e-Ahl-e-Sunnat  
Muasisi wa Dawat-e-Islami, Allamah Maulana Abu Bilal

**MUHAMMAD ILYAS**  
Attar Qadiri Razavi

تاسیس کنندہ  
ابو بلال



مکتبۃ المدینہ  
MAKTABA AL-MADINA  
MC 1286

صبح بہاراں

Subh-e-Baharan



# Upambazuko Wa Asubuhi



Kitabu hiki kiliandikwa na Shaykh-e-Tariqat Amīr-e-Ahl-e-Sunnat, muanzilishi wa Dawat-e-Islami ‘Allāmah Maulānā Abu Bilal Muhammad Ilyas Attar Qadiri Razavi دامت بركاتهم العالیة Katika lugha ya Kiurdu. Kimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na Majlise Tarajim. Endapo utaona makosa yoyote katika tafsiri yake au utungaji wake, tafadhali wasiliana na Majlise Tarajim kwa njia ya posta au kwa kipepesi ili upate thawabu.

## Majlis-e-Tarājim (Dawat-e-Islami)

Aalami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah, Mahallah Saudagran,  
Purani Sabzi Mandi, Bab-ul-Madinah, Karachi, Pakistan

UAN: ☎ +92-21-111-25-26-92 – Ext. 1262

Email: ✉ translation@dawateislami.net

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ عَلَى سَيِّدِ الْمُرْسَلِينَ  
أَمَّا بَعْدُ فَأَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

## Dua Kabla Ya Kusoma Kitabu

Kabla ya kusoma kitabu au somo la kidini, soma dua ifuatayo.  
Insha-Allah عَزَّوَجَلَّ utakumbuka yote uliyoyasoma.

اللَّهُمَّ افْتَحْ عَلَيْنَا حِكْمَتَكَ وَأَنْشُرْ  
عَلَيْنَا رَحْمَتَكَ يَا ذَا الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ

Ee mola عَزَّوَجَلَّ Ifungue milango ya elimu na busara kwa ajili yetu, na utuhurumie! Ewe ulie mtakatifu kabisa.

*(Al-Mustatraf, vol. I, pp. 40, Dar-ul-Fikr, Beirut)*

**Kumbuka:** Mswalie Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ mara moja kabla na baada ya dua.

# Yaliyomo

Dua Kabla Ya Kusoma Kitabu.....ii

## Upambazuko Wa Asubuhi.....1

Fadhila za kumsalia Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ .....	1
Pambazuko la asubuhi.....	2
Muujiza.....	3
Usiku wenye fadhila zaidi kuliko usiku wa Shab-e-Qadr .....	4
Sikukuu bora kuliko sikukuu zote .....	5
Abuu Lahab na maulidi.....	5
Waislamu na maulidi.....	6
Tusherekee kwa shangwe uzawa wa Mtume .....	6
Wenye kufurahia Uzawa wa Mtume na yeye pia humfurahia .....	7
Furaha wa Uzawa wa Mtume pamoja na bendera.....	7
Zafa pamoja na bendera .....	8
Ukoo ulio sherekea Uzawa wa Mtume.....	8
Thawabu ya kuadhimisha Uzawa wa Mtume .....	12
Wayahudi wamebahatika kupata imani.....	12

Dawat-e-Islami na Uzawa wa Mtume ..... 15

Nimepata tiba ya ugonjwa wa dhambi..... 15

Uchafu wa roho umesafishika ..... 16

Mvua ya nuru..... 17

Hata leo miujiza inaonekana ..... 19

Kwa niaba ya herufi kumi na mbili ya marhaba ya Mustafa  
kwa kusherekea Uzawa wa Mtume.....21

Barua ya Attar inayo husiana na uzawa wa Mtume .....25

Tahadhari .....28

Nia ya kusherekea maulidi.....33

Kwa niaba ya herufi 18 za marhaba uzawa wa Mtume na nia  
18 za kusherekea.....34

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ عَلَى سَيِّدِ الْمُرْسَلِينَ  
أَمَّا بَعْدُ فَأَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

# Upambazuko Wa Asubuhi



**Fadhila za kumsalia Mtume** صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

Agizo la mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ anasema mwenye kunisalia mara kumi (10) Allah عَزَّوَجَلَّ atamteremshia rehma mia moja.

*(Al-Mu'jam-ul-Awsat lit-Tabarānī, Vol. 5, pp. 252, Ḥadīṣ 7235)*

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

Mwezi Mtukufu wa Rabi-ul-Noor Shariff unapoingia kila mahali msimu unakuwa mzuri, wapenzi wa mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ si vijana si wazee, kila moja wao hufurahia, kwa hakika nyoyo zao na ndimi zao husema *marhaba ya mustafa* .

*Nišār tayrī chaḥal paḥal per ḥazār Eidayn Rabī’-ul-Awwal  
Siwāye Iblīs kay jahān mayn sabḥī to khushiyān manā raḥay ḥayn*

Wakati ulimwengu ulipotanda giza ya shirk, kufu na dhulma, ilipoingia tarehe 12 Mwezi Mtukufu wa Rabi-un-Noor Sahriff katika Mji wa Makka-Tul-Mukarrama nyumbani kwa Hazrat Sayyidatuna Amina رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهَا mama yetu, ilimeremeta nuru ya Mtume wetu Mtukufu wa Daraja صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na kuleta mwanga Ulimwengu mzima na kuondoka kwa dhulma, shirk na kufu.

*Mubārak ḥo kay Khatm-ul-Mursalīn tashrīf lay āye  
Janāb-e-Raḥmat-ul-lil-‘Ālamīn tashrīf lay āye*

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

## **Pambazuko la asubuhi**

Mtume wetu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Alipozaliwa tarehe 12 nyakati za kupambazuka alikuja na rehema kwa ajili ya wale walio kuwa wana dhulumiwa, kuteswa na kwaajili ya wale wanaohangaika na kuwaletea manufaa.

*Musalmāno Ṣubḥ-e-Baḥārān mubārak  
Woh barsātay anwār Sarkār صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ āye*

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

## Muujiza

Mnamo tarehe 12 Mwezi wa Rabi-un-Noor Shariff ilipokuja Nuru ya Mtume wetu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ulimwenguni. Mawingu ya dhulma na shirki yalijificha na nyumba ya mfalme Shaahe Iran kisra ulikuja mtetemeko na kuangusha nakshi 14 na pia kuzimika kwa moto uliokuwa ukiwaka kwa miaka 1000, Mto Sawah ulikauka na Al-Kaaba ilitingishika na kuangusha sanamu.

*Tayrī āmad thī kay Baytullāh mujray ko jhūkā  
Tayrī haybat thī kay har but thar tharā kar gir gayā*

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Nabii wa Rehma Shafii wa Umma Mtume wetu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alipokuja duniani alikuja na fadhila na Rehma na hakika siku ambayo ili teremka Rehma ya Allah عَزَّوَجَلَّ ndio siku ya kufurahia na kusherekea. Allah عَزَّوَجَلَّ Anasema ndani ya Qur'an:

قُلْ بِفَضْلِ اللَّهِ وَبِرَحْمَتِهِ فَبِذَلِكَ فَلْيَفْرَحُوا هُوَ خَيْرٌ مِمَّا يَجْمَعُونَ ﴿٥١﴾

**TAFSIRI YAKE:** Kwa fadhila ya Allah-mtukufu (yaani Uislamu) na kwa rehma yake (yaani Mtume Muhammad صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Au Qur'an Tukufu) basi, kwa hizo wewe (yaani fadhila na rehma) ndio wao (waislamu) wanapaswa kufurahia Hilo (la kufurahia) ndio kheri zaidi (kwao) kuliko (kufurahia) vile vyote wanayokusanya (katika mali na watoto



hapa Duniani). [Kanz-ul-Īmān (Translation of Quran)] (Part 11, Sūrah Yūnus, Verse 58)

اللَّهُ أَكْبَرُ! Qur'an tukufu inatusisitiza kwa kufurahia Rehma za Allah عَزَّوَجَلَّ je kuna neema inayo zidi kuliko kuja kwa mtukufu wa daraja Mtume wetu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَالْوَالِدِينَ وَسَلَّمَ . . Sikia ilani wazi wazi ndani ya Qur'an tukufu.

وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِّلْعَالَمِينَ ﴿١٠٧﴾

**TAFSIRI YAKE:** Na hatukukutuma wewe Muhammad isipokuwa uwe heshima kwa walimwengu.

[Kanz-ul-Īmān (Translation of Quran)] (Part 17, Sūrah Al-Anbiyā, Verse 107)

## Usiku wenye fadhila zaidi kuliko usiku wa Shab-e-Qadr

Mwanazuoni Hazrat Sheikh Abdul-Haq Dhelvi عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْقَوِي أَناسема:-Hapana shaka Uzawa wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَالْوَالِدِينَ وَسَلَّمَ ni siku bora kuliko usiku wa Lailla-tul-Qadar,kwa kuwa usiku wa Uzawa wa Bwana Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَالْوَالِدِينَ وَسَلَّمَ nisiku ya kuja kwake Duniani na wakati Lailla –tull- Qadar alijaliwa Mtume na usiku ambao uli pata utukufu kwa kushuka kwa Malaika.

(Māšabata bis-Sunnah, pp. 100)

## Sikukuu bora kuliko sikukuu zote

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ! Kwajili ya waislamu tarehe 12 ya Rabi-ul-Noor Shariff ni sikukuu bora kuliko sikukuu zote hakika Nabii wa Rehma Shafii wa Umma صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّمَ Asinge kuwepo basi Iddi ya aina yeyote ile isinge kuwepo hata hiyo Lailla-tul-Qadar pia isinge kuwepo, hayo yote yamepatikana kwa niaba yake.

*Woh jo na thay to kuch na tha woh jo na haun to kuch na ho  
Jan hayn woh jahān kī, jān hay to jahān hay*

صَلُّوْا عَلٰى الْحَبِيْبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلٰى مُحَمَّدٍ

## Abuu Lahab na maulidi

Wakati Abuu Lahab alipofariki baadhi wa watu wake wa nyumbani walimuota ndoto mbaya na kumuuliza umepata nini? Akasema baada ya kuachana na nyinyi siku bahatika kupata kheri ya aina yeyote na kisha akaonesha ishara kwenye tundu la dole gumba na kusema nina nyweshwa maji kwasababu mimi nilimwachia huru mtumwa (Suwaiba).

*(Muṣannaf ‘Abdur Razzāq, Vol. 9, pp. 9, Ḥadīṣ 16661) (‘Umda-tul-Qārī, Vol. 14, pp. 44, Ḥadīṣ 5101)*

Shaykh ‘Allāmah Badruddīn ‘Aynī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللهِ الْقَوِي Anasema: Maana ya ishara ni mimi ninapata maji kidogo ya kunywa.

*(‘Umda-tul-Qārī, Vol. 14, pp. 44, Ḥadīṣ 5101)*

## Waislamu na maulidi

Kutokana na riwaya hii Sayyidunā Shaykh ‘Abdul Ḥaq Muḥaddiṣ Dihlvi عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْقَوِي Anasema: Kuna dalili kubwa kwa watu wanao adhimisha Uzawa wa Mtume صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Kwa furaha na kutumia mali na pesa zao. Kwani mtu kama Abuu Lahab aliye kuwa Mkafiri aliposikia Uzawa wa Mtume صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Kwa furaha alimwachia huru Mtumwa wake (Suwaiba) kwa ajili ya kuenda kumnyonyesha na akapata jaza’ yake.

Jaza’ ya yule ambae anasherekea na kutumia mali na pesa zake kwa ajili ya mahaba ya Uzawa wa Mtume صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na kupata ridhaa ya Allah عَزَّوَجَلَّ atakuwa kwenye daraja gani, lakini zingatia usisherekee kwa kupiga ngoma na muziki.

*(Madārij-un-Nubūwwah, Vol. 2, pp. 19)*

## Tusherekee kwa shangwe uzawa wa Mtume

Wapenzi watukufu waislamu, Tusherekee kwa shangwe na furaha Uzawa wa Mtume صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Wakati Mkafiri kama Abuu Lahab alifurahia na akapata faida siyo kwa ajili ya Mtume bali kwa ajili ya kupata Mjukuu na sisi الْحَمْدُ لِلَّهِ عَزَّوَجَلَّ Waislamu tukisherekea kwa ajili ya ridhaa ya Allah عَزَّوَجَلَّ Uzawa wa Mtume Mtukufu wa Daraja Mfalme wa Makka na Madina Mtume wetu صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kwa nini tusifaidike?

*G̃har Āminah̃ kay Sayyid-e-Abrār ā gayā*

*Khushyān manāo ghamzado Ghamkhuwār ā gayā*

## Wenye kufurahia Uzawa wa Mtume na yeye pia humfurahia

Mwana zuoni moja رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ Anasema: مُحَمَّدٌ لِلَّهِ عَزَّوَجَلَّ Mimi nimefanya ziara ya Mtukufu wa Daraja Nabii wa Rehma Shafii wa Umma Mtume صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kwenye ndoto na kumuuliza Ya Rasulallah صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ! je wewe unafurahia waislamu kila mwaka wanasherekea Uzawa wako? Akasema: Wale wanaonifurahia Mimi, Mimi pia nawafurahia wao.

*(Tazkira-tul-Wā'izīn, pp. 600)*

## Furaha wa Uzawa wa Mtume pamoja na bendera

Sayyidatuna Amina رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهَا Anasema: Mimi nimeona bendera tatu zimewekwa:

- ❖ Moja mashariki
- ❖ Ya pili magharibi
- ❖ Tatu juu ya Al- Kaaba
- ❖ Na kisha Mtume صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Amezaliwa. *(Khasāiṣ-ul-Kubrā, Vol. 1, pp. 82)*

*Rūḥ-ul-Amīn nay gā'ā Ka'bay kī chāt pay jhāndā  
Tā 'Arsh u'rā p̄harayrā subḥ-e-shab-e-wilādat*

## Zafa pamoja na bendera

Nabii wa Rehma Shafii wa Umma Mtume wetu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Alipofanya hijra kutoka mji mtukufu wa Makka tul- Mukarrama na kuelekea mji wa Madina-tul-Munawwara, alipofika karibu na mji wa (Mauzih Ghamim) Bureida Aslami kabila ya Banii Saham alikuja na msafara wa watu 70 ili kumkamata. Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Baada ya kuona macho Matukufu ya Mtume wetu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Alinyenyekeka na kuingia kwenye dini ya Uislamu pamoja na watu sabini (70) na akasema: Ya Rasulallah! sasa utaingia kwenye mji wa Madina pamoja na bendera na shangwe na kisha akavua kilemba chake na kukifunga kwenye mkuki na kutangulia mbele ya Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na kuongoza msafara. (*Wafā-ul-Wafā, Vol. 1, pp. 243*)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

## Ukoo ulio sherekea Uzawa wa Mtume

Katika Mji wa Madina-tul-Munawara Alikuwapo mja,kwa jina aliitwa Ibrahim. Aliyekuwa Mpenzi wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Siku zote alikuwa akitafuta Rizki yake, kwa njia ya halali, na nusu ya mapato yake huweka mbali kwa ajili ya kusherekea Uzawa wa Mtume Wetu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kila ifikapo mwezi mosi wa Rabi-ul-Noor Shariff<sup>1</sup>. Basi Husherekea kwa shangwe

---

<sup>1</sup> Laiti ingewezekana hisa moja ya mapato yetu tunge weka mbali kwa ajili ya Maulidi ama kwa ajili ya kazi njema yeyote ya dini.

kwa kuzingatia sheria. Pia hufunga swaumu, hutoa sadaka kwa ajili ya Mtukufu wa Daraja na kutumia pesa kwa ajili ya kazi njema, Mke Wake pia alikuwa mpenzi wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na akishirikiana naye kiukamilifu shughuli zote. Mke wake alipofariki hakuwa na mabadiliko kwenye ratiba yake.

Mpenzi Ibrahim siku moja alimwita mtoto wake na kumuusia. Mwanangu mpenzi usiku wa leo mimi nitafariki, kwenye akiba yangu nina dhirham hamsini, na nguo ambayo utaitumia kwa ajili ya sanda yangu ipotayari. Na ile Dhirham Hamsini, utaitumia kwa ajili ya kazi njema. Baada ya kusema hayo alisoma Qalima na roho yake ilitoka. Mtoto kwa mujibu wa wosia wa baba yake alimzika, lakini Dhirham Hamsini (50) hakujua aitumie kwenye kazi gani njema.

Alipokuwa na fikra hii, aliota ndoto Qiana imesha simama, kila moja wetu yuko kwenye hali ya kuokoa nafsi yake, Watu wema wanaingia peponi, na watu wabaya wanabururwa na kusukumwa ndani ya moto. Yeye alisimama na kutetemeka, hajui uamuzi wake utakuaje kwa ajili yake. Ghafla akasikia nidaa ikisema muacheni huyu kijana aingie peponi. Kijana alifurahi na kuingia peponi na kuanza kuzunguka pepo.

Baada ya kuzunguka pepo (7) alipofika kwenye pepo ya nane alimkuta askari wa pepo Hazarat Ridhwan na akasema kwenye pepo hii wanaingia wale ambao wamesherekea Maulidi ya Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Katika Mwezi wa Rabi-ul-Noor Shariff. Hapo hapo kijana akaelewa kuwa marehemu Wazazi

wangu watakuwa humu, ghafla ikasikika sauti ikisema, muacheni huyu kijana aingie, Wazazi wake wanataka kuonana nae. Alipoingia ndani alimkuta Mama yake Mzazi amekaa karibu na Mto Kauthar, na juu ya mto limewekwa jukwaa, ambayo amekaa Malkia wa pepo, na vimepangwa viti kando kando yake, ambao baadhi ya akina mama wamekaa na sura zao zinameremeta na kung'ara na nuru.

Yule kijana akamuuliza Malaika moja, akina Mama hao ni nani? Malaika akasema aliyekaa juu ya jukwaa ni Malkia Saidatuna Fatma-tu-Zahra رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهَا na juu ya viti mama Khadhija-Tul-Qubra, Aisha Sidiqa, Saidatuna Maryam, Sayyidatuna Asia, Sayyidatuna Sarah, Sayyidatuna Hajra, Saida tuna Rabia na Saidatuna Zubeda رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُنَّ.

Kijana alifurahi sana na kuendelea mbele na akaona jukwaa moja lililopambwa vizuri sana na juu yake amekaa mtukufu wa Daraja Mfalme wa Dunia na Akhera Nabii wa Rehma Shafii wa Umma Mwenye Taji la Madina صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Ambae uso wake Mtukufu ulio kuwa ukimeremeta kama mbala mwezi na jirani yake vime zungushwa viti winne ambavyo wamekalia Khulafā-e-Rāshidīn عَلَيْهِمُ الرِّضْوَانُ Upande wa kulia vimepangwa viti vya Dhahabu na wame kaa Anbiya-e-Kiram عَلَيْهِمُ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ Na kushoto vimepangwa viti ambavyo wamekalia Shuhadaa kiram na ghafla akamuona Baba yake yuko katika kikao Tukufu cha Bwana Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na kisha Baba yake alipomuona alimkumbatia na kijana alifurahi sana na kumuliza swali je baba umepataje daraja hili adhimu?

Akamjibu hayo yote nimepata kutokana na kusherekea Uzawa wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ baada ya hapo macho yake yakafunguka. Uzawa wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ baada ya hapo macho yake yakafunguka

Kulipo pambazuka aliuza nyumba yake kwa bei ndogo na kuchukua pesa na kujumlisha dhirham hamsini aliye achiwa na marehemu baba yake kisha akachukua jumla ya zile pesa na kuandaa tafrija ya kuwaalika Mashekhe na kuwalisha chakula. Kisha moyo wake haukuipenda Dunia bali alienda kufanya ibada Msikitini na kuhudumia Msikiti kwa muda wa miaka 30 alipofariki Mja Mmoja alimuona kwenye ndoto na kumuuliza ilikuaje na wewe? Akajibu kwa Baraka ya kusherekea Uzawa wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Wamenipeleka Peponi kwa marehemu Baba yangu. (*Taḏkira-tul-Wā'izīn*, pp. 557)

Iwe rehma ya Allah عَزَّوَجَلَّ juu yake na kwa niaba yake iwe maghufira yetu.

أَمِينَ بِجَاهِ النَّبِيِّ الْأَمِينِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

*Bakhsh day mujh ko Ilāhī! Bah̄r-e-Milād-un-Nabī  
Nāmah̄-e-a'māl 'iṣyān say mayrā bh̄arpūr hay*

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ



## Thawabu ya kuadhimisha Uzawa wa Mtume

Shaykh ‘Abdul Ḥaq Muḥaddiṣ Dihlvī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْقَوِي Anasema: Jazaa ya yule, anayeadhimisha Uzawa wa Mtume صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Allah عَزَّوَجَلَّ Kwa Fadhila yake na Ukarimu wake Allah عَزَّوَجَلَّ Ata waingiza kwenye Pepo ya Janna-tul-Naeem. Waislamu huwa wanaadhimisha Uzawa wa Mtume صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Wanasoma Maulidi, wana andaa karamu ya kuwalisha watu chakula, wanatoa sadaka, wanafanya karama nyingi, wanapamba nyumba zao, wanafanya gharama nyigi kwa ajili ya Uzawa na kufurahia. Kwa hayo yote kazi njema Allah عَزَّوَجَلَّ Hushusha Rehema zake kwa waja wake. (*Māṣabata bis-Sunnah*, pp. 102)

## Wayahudi wamebahatika kupata imani

Sayyidunā ‘Abdul Wāḥid Bin Ismā‘īl عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْجَمِيل Anasema: Katika Mji wa Misri alikuwepo mja moja wa mpenzi wa Mtume صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ambae kila ifikapo mwezi wa Rabi-ul-Noor Shariff kwa ajili ya kipenzi cha Allah عَزَّوَجَلَّ Anaadhimisha Uzawa wa Mtume صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ.

Safari moja mwezi wa Rabi-ul-Noor Shariff, jirani yake Myahudi akamuuliza Mume wake, huyu jirani yetu Muislamu kwanini anawaalika watu hasa mwezi huu? Myahudi akamjibu ndani ya mwezi huo amezaliwa Nabii wake صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kwa hiyo, kwa ajili ya furaha anafanya tafrija na kuwaalika

Waislamu kuja kusherekea Uzawa wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَالْوَالِدِينَ وَسَلَّمَ na Waislamu wana heshimu sana mwezi huo.

Mke wake Myahudi akasema: Waislamu wana tabia nzuri sana ya kuadhimisha kila mwaka Uzawa wa Mtume wao صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَالْوَالِدِينَ وَسَلَّمَ. Usiku alipo lala mke wake, aliota ndoto yakuwa mja moja mwenye kiumbile mzuri sana, na mweupe sana, akiwa na watu jirani yake na kufika kwake. Yule Myahudi akasogea mbele na kumuuliza mja moja, huyu ni nani? Akamjibu: Huyu ni Nabii wa mwisho, Nabii wa Rehma Shaffii wa Umma na ni Rehma kwa ajili ya walimwengu wote صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَالْوَالِدِينَ وَسَلَّمَ Na kuja kwake hapa ni kwa ajili ya jirani yako Muislamu kumpa Kheri na Baraka, kwa ajili ya kuadhimisha Uzawa wa Mtume na kuonana nae.

Yahudi akamuuliza je Mtume wako صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَالْوَالِدِينَ وَسَلَّمَ Atanijibu swali langu? Yule akajibu ndiyo. Yahudi akamwita Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَالْوَالِدِينَ وَسَلَّمَ Akamjibu Labaik, Myahudi akashangaa na kusema mimi si Muislam lakini Nabii صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَالْوَالِدِينَ وَسَلَّمَ Akanijibu Labaik Nabii wa Rehma Shaffii Wa Umma صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَالْوَالِدِينَ وَسَلَّمَ Akasema: Nimepata bishara kutoka kwa Allah عَزَّوَجَلَّ Kuwa wewe utaingia kwenye Dini ya Uislamu alipiga kite na kusema: Hapanashaka wewe ni Nabii wa Rehma Shaffii wa Umma صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَالْوَالِدِينَ وَسَلَّمَ Na mwenye Ukarimu

Yule mwenye kukuudhi wewe ataangamia na yule asiye kutukuza yuko kwenye khasara. Yaani mwenye kubeba hasara] na kisha akatoa shahada na kusoma Qalima. Kisha macho yake yalipo funguka alikubali Uislamu kwa moyo moja, na kunuia kuwa patakapo kucha mali yangu yote nitaitumia kwa ajili ya kipenzi cha Allah **عَزَّوَجَلَّ** Kwa kuadhimisha Uzawa wake na nitafanya Tafrija. Alipo amka asubuhi alimkuta Mume wake anatararisha maandalizi ya kuwaalika watu na yeye alishangaa na kumuuliza wewe unafanya nini? Akamjibu: Mimi ninafuraha ya kuwa wewe umekubali Uislamu na mimi ninaandaa Tafrija. Mke wake akamuuliza wewe umejuaje? Akajibu: mimi pia nimeoteshwa ndoto na nikakubali Uislamu katika mkono Mtukufu wa Bwana Mtume **صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ**. (*Tazkira-tul-Wā'izīn*, pp. 598)

Iwe Rehma ya Allah **عَزَّوَجَلَّ** juu yake na kwa niaba yake iwemaghufira yetu.

أَمِينٌ بِجَاهِ النَّبِيِّ الْأَمِينِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

*Āmad-e-Sarkār say zulmat hūī kāfūr hāy  
Kyā zamīn, kyā āsmān hār samt chāyā Nūr hāy*

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

## Dawat-e-Islami na Uzawa wa Mtume

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ! Dawat-e-Islami Ni [Shirika la kimataifa la kueneza mafundisho ya Qur'an na Sunna lisilo jihusisha na siasa] Dawat-e-Islami huadhimisha Uzawa wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kwa aina yake pekee ulimwenguni. Dawat-e islami inasherekea Uzawa wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kwa kuanda ijtimah kutoa Bayaan, kusoma Qasida na Kuzukuru. Katika Ulimwengu, upande wa Karachi eneo la Babul Madina inakuwa Ijtimah kubwa sana kuliko sehemu nyingine ya ulimwengu. Tutaongelea nini Baraka zake, Wanao bahatika kushiriki humo hupata mabadiliko ndani ya maisha yao. Hebu tupate maua manne ya kimadani .

## Nimepata tiba ya ugonjwa wa dhambi

Mpenzi moja wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ anaeleza hivi: usiku wa kusherekea Uzawa wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ulivyo andaliwa na taasisi za Dawat-e-Islami kwenye uwanja wa Kakri Ground Babul Madina Karachi alikua kijana moja aliyehudhuria, Ambaye asiye Swali, aliye kuwa kijana wa kisasa.

Ilipo fika alfajiri muda wa Uzawa wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ watu walipoanza kumswalia Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Na kusikia kwa Marhaba ya Mustafa kijana Yule asiyeswali moyo wake ulilainika na kubadilika na kuelekea upande wa kheri na kuchukua maasi na hapo kwa papo ameanza kuswali na kunuia kupamba ndevu na kwa hakika amekuwa mswalihina. Alikuwa na ubaya moja ndani mwake lakini haina haja ya kuelezea.

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ kwa Baraka ya Ijtimah ya Dawat-e-Islami ubaya wake pia uliondoka. Kwa maneno mengine tunaweza kusema kwa Baraka ya ijtimah na zikri maradhi ya maasi yanatoka na ukapata tiba.

*Māng lo māng lo un kā gham māng lo*

*Chashm-e-rahmat nigāh-e-karam māng lo*

*Ma'siyat kī dawā lā-jaram māng lo*

*Māngnay kā mazā āj kī rāt hāy*

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

## Uchafu wa roho umesafishika

Ndugu moja wa eneo la upande wa kazkazini ya Karachi anaandika hivi: Mwanzoni mwa mwezi wa Rabi-ul-Noor Sharif baadhi ya wapenzi wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Waliniling'ania niende nao kwenye ijtimah nakusherekea Uzawa wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Itakayo fanyika tarehe 12 ya Rabi-ul-Noor kwenye uwanja wa Kakri eneo la Babul Madina Karachi itakayo andaliwa na Tasisi ya Dawat-e-Islami bahati yangu nzuri mimi niliwakubalia, ifikapo tarehe mimi nitakuja.

Kwa mujibu wa ahadi niliyo itoa nilienda kujumuika na wapenzi wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Ili niweze kusafiri nao kwenye Madani Qafilah kwa ajili ya kusherekea Uzawa wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na ijtimah. Tulipokaa ndani ya basi na

kuanza safari za Madani Qafilah mpenzi moja wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Alitoa tabaruk na kuwagawia waislamu karibu 30 kidogo kidogo kijana aliye kuwa anagawa tabaruk kwa moyo safi ilinigusa sana na hadi sisi tumefika kwenye ijtimah, Mimi nimeona mara yangu ya kwanza katika maisha yangu jinsi wanavyo soma Qasida na kumswalia Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Hadi uchafu wa roho yangu ulisafishika,

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ Hapo kwa papo nilijiunga na Taasisi ya Dawat-e-Islami na kuweka nia ya kupamba ndevu na kuvaa kilemba rangi ya kijani na wakanipa jukumu la kuwa amiri wa eneo na kufanya kazi za kimadani na kueneza Sunna ya Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ.

*'Aṭā-e-Ḥabīb-e-Khudā Madanī Māḥaul*  
*Ḥay fayzān-e-Ghauṣ-o-Razā Madanī Māḥaul*  
*Yaqīnan muqaddar kā woḥ ḥay sikandar*  
*Jisay khayr say mil gayā Madanī Māḥaul*

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

## Mvua ya nuru

Mwaka 1417 Hijria wakati wa dhuhuri kama kawaida ya kila mwaka baada ya swala ya dhuhuri zafa ya Dawat-e-Islami ilianza kutoka kitongoji cha Nazima-Baad Babul Madina, Karachi ilianza kwa shangwe kubwa kwa kusoma Marhaba ya

Mustafa na kupita mitaani. Ilipokuwa inapita sehemu mbalimbali na kuwa alika watu kwa ajili ya dawa njema. Sehemu moja kijana moja asiye pungua umri wake miaka kumi aliwaalika watu kwa ajili ya dawa njema. Wakati anapo waalika zafa yote ilitulia na kusikiliza kijana mdogo anavyo waalika watu.

Baada ya kumalizika kwa bayaan mtu moja aliinuka na kuwauliza watu na kufika kwa Amiri wa zafa na kumueleza yakuwa mimi nimeona kwa macho yangu wakati wa bayaan kijana mdogo pamoja na watu walio shiriki kwenye zafa ilikuwa inawanyeshea mvua ya nuru, Anasema naomba utanisamehe kwa vile mimi sio muislamu naomba tafadhali niingizeni kwenye dini ya uislamu haraka.

Baada ya kusikia marhaba ya Mustafa kifua changu kimeleinika. Sikukuu ya kuadhimisha Uzawa wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na kwa niaba ya Dawat-e-Islami Shetani atakuwa anagonga kichwa chake. Baada ya kuingia kwenye Uislamu Yule mja anasema: إِنَّ شَاءَ اللهُ عَزَّوَجَلَّ Mimi nitaingiza ukoo wangu wote kwenye uislamu kwa kweli Yule alifanya hivyo hivyo na kwa Baraka ya kuwaling'ania mke wake na Watoto wake watatu na Mzazi wake walikubali Uislamu.

*Koī āyā pā kay chalā gayā, koī 'umar bhār bhī na pā sakā  
Yeḥ baḥay karam kay ḥayn faīṣlay, yeḥ baḥay naṣīb kī bāt ḥay*

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

## Hata leo miujiza inaonekana

Mpenzi moja wa Mtume ﷺ Anasema hivi: Siku hizi maandalizi yanayo andaliwa na Taasisi ya Dawat-e-Islami Kwenye uwanja wa Kakri ambayo ni kubwa kuliko sehemu nyingine ya Ulimwengu lakini haina raha kama zamani.

Mwenzake akamjibu: Unakosea kwani Zikri ni ileile bali nyoyo zetu zime badilika, Itawezekanaje Zikri ya Mtume ﷺ Ibadilike,ni sisi mawazo yetu yamebadilika, hata hapo tulipo badala ya kuleta fikra ya hapo na pale na tungetulia kuwaza ubora wa Mtume ﷺ Na tukasikia Qasida kwa makini basi *إِنْ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ* tutapata faida juu ya faida.

Moja kati yao Shetani alimghalibu na kumshawishi kurudi nyumbani kwake lakini jawabu ya mwenzake ilikuwa nzuri sana ya kuiamsha (nafsilawama) na kumkimbiza Shetani. Marhaba jawabu alionipa iliniingia moyoni na mimi niliingia ndani ya ijtimah na kujumuika na wenzangu, Nilipo zama kiundani na fikra na kukaa na wapenzi wa Mtume ﷺ na kusikia Qasida ilipokaribia nyakati za alfajiri muda wa mtukufu wa daraja anapozaliwa wapenzi wa Mtume ﷺ waliposimama kwa ajili ya kiamu kila kona ilisikika kwa vishindo marhaba, marhaba marhaba ya Mustafa, na wakimswalia Mfalme wa Makka na Madina Mtukufu wa Daraja Mwenye Taji la Madina ﷺ.



Wapenzi wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ yaliwatoka machozi ya furaha na mimi ilinigusa sana macho yangu yenye dhambi yaliona marasharasha ya mvua na hali ya hewa ilibadilika kwa hakika nilikuwa ninaoagelea kwenye Rehma ya Mwenyezi Mungu pamoja na wanaijtimai wote nilifunga macho yangu na kuwaza uzuri wa Mtukufu wa Daraja صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na kumswalia hapo kwa papo macho yangu ya moyo yalifunguka. Nasema kweli pindi niliposherekea Uzawa wa Mtukufu wa Daraja Mfalme wa Makka na Madina Mtume wetu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ mimi mwenye dhambi. kwa macho yangu nimeona manyunyu za mvua na wanaijtimai wote wanaoagelea katika mvua ya rehma. Mimi nilifunga macho yangu na kuzama kuwaza uzuri wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na kumswali Mtukufu wa daraja. Ghafla macho yangu ya moyo ulifunguka, nina sema kweli Yule ambae tunamshereka Uzawa wake.

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ Nilijaliwa Karama na kufanya Ziara ya Mtume wetu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Baada ya kufanya Ziara ya Mtukufu wa Daraja Mtume wetu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ moyo wangu ulikua umefurahi sana. Hakika mwenzangu aliniambia ukweli kabisa yakua ijtimah ya Dawat-e-Islami iko vilevile bali nafsi zetu zimebadilika kwa hakika kama sisi nyoyo zetu zikiwa halisi basi hata leo tunaweza kuona Karama nyingi.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

## Kwa niaba ya herufi kumi na mbili Uzawa wa Mustafa Maua kumi na mbili ya kusherekea Uzawa wa Mtume

- ❖ Kuna maua kumi na mbili ya kimadani: Kwa ajili ya furaha wa Uzawa wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Tupeperushe bendera Msikitini, majumbani, madukani, mitani na katika magari, zenye rangi ya kijani kibichi. Tunga'rishe kwa kuweka taa nyingi katika maeneo na mitani. Nyumbani kwako usikose japo uweke balbu 12 kwa niaba ya tarehe 12 ya Rabi-ul-Noor Shariff. Unuie kwa ajili ya kupata thawabu ujumuike katika ijtimai ya Dawat-e-Islami, na ifikapo muda wa Uzawa wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Usimame kwa taadhima na huku uchukue bendera na kuipeperusha na kumswalia Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kwa nia ya kupata thawabu. Na ikiwezekana tarehe 12 ufunge swaumu kwa vile Mtume wetu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Alikuwa anaadhimisha siku ya jumatatu ya kuzaliwa kwake kwa kufunga swaumu. kama jinsi:

Hazrat Seyyiduna Abu Qatadha رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ Anasema katika ukumbi wa Mtume alimuuliza mtukufu wa daraja mwenye taji la Madina Mtume wetu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kuhusiana na swaumu ya jumatatu. Nabii wa rehma shafii wa umma Mtukufu wa Daraja Mfalme wa Makka na Madina akajibu kuwa nimezaliwa siku ya jumatatu na iliteremshwa wahii juu yangu siku hiyo.

*(Ṣaḥīḥ Muslim, pp. 591, Ḥadīṣ 198)*

Sharii Sahii Bukhari Hazrat Sayyiduna Imam Kastalani رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ Anasema: Yule mwenye kuandaa Uzawa wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Kwa hakika Yule ana kaa kwa amani na jambo hilo wengi wamethibitisha na pia kazi zake humalizika kwa wepesi.

Allah عَزَّوَجَلَّ Amteremshie Rehma Yule aliye sherekea usiku wa Uzawa wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na kufanya sikukuu. *(Al-Mawāhib-ul-Ladunniyah, Vol. 1, pp. 148)*

- ❖ Kutufu Al-Kaaba na madoli Mwenyezi Mungu atunusuru. Huonekana kwa kutufu na madoli ni dhambi. katika dhama ya ujinga palikuwa na madoli yaani sanamu zilizo wekwa ndani ya Al-Kaaba inayo fika idadi ya 360. Baada Ya Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kuigomboa Al-Kabaa alitoa sanamu zote na kusafisha Al-Kabaa kwa hivyo haitakiwi tena kuwa na madoli wala sanamu ndani ya Al-Kaba nafasi yake tunaweza kuweka maua ya plastiki. Tunaweza kuweka hata Miskitini au majumbani picha ya Al-Kaaba ambayo wakati watu wanapoitufu (kuzunguka) lakini zisionekane nyuso zao waziwazi kwani imekatanzwa na ni dhambi nausiweke fremu yenye kuonyesha uso hata kama umesimama kwa mbali na inaonekana imekatanzwa na ni dhambi.

- ❖ Pia tunakatazwa kuweka picha za wanyama mfano amechorwa tausi nakadhalika na kupamba juu ya mageti.  
**Hadithi mbili zinazo husiana na picha za Wanyama .**
  - i. Malaika wa rehma hawaingii kwenye nyumba yenye Mbwa na picha za Wanyama.  
*(Ṣaḥīḥ Bukhārī, Vol. 2, pp. 409, Ḥadīṣ 3322)*
  - ii. Yule mwenye kuchora kitu chenye uhai Allah عَزَّوَجَلَّ atakuwa atampa adhabu mpaka apulize roho ndani mwake na hilo halito wezekana.  
*(Ṣaḥīḥ Bukhārī, Vol. 2, pp. 51, Ḥadīṣ 42)*
- ❖ Kwa kusherekea uzawa wa Mtume kwa muziki na ngoma ni dhambi sikia riwaya mbili:
  - i. Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ anasema nimepata hukumu ya kuvunja matarumbeta na ngoma.  
*(Firdaus-ul-Akḥbār, Vol. 1, pp. 483, Ḥadīṣ 1612)*
  - ii. Kuna riwaya kutoka kwa Hazrat Seyyiduna Zahaq muziki ina haribu nyoyo na ina muudhisha Allah عَزَّوَجَلَّ. *(Tafsīrāt-e-Aḥmadiyyah, pp. 603)*
- ❖ Hapana shaka unaweza kusikia kanda za qasida kwa sauti ndogo kwa kuzingatia wale walio lala, wagonjwa na kwa wale wanao Swali na pia uzingatie Azana na Swala. Usilize kasida zilizoimbwa na mwanamke.

- ❖ Pia usije ukapamba barabara kwa kuweka mabendera na nguzo kisha waendesha magari na wapita njia waka pata matatizo ni dhambi.
- ❖ Hairuhusiwi Wanawake hutokeza kwa kuangalia taa na mapambo na huja mbele ya wanaume ni tendo la haramu kwa vile huja wamejipodoa nakusababisha wanaume ishki ni jambo la kusikitisha na pia uzingatie si ruksa ya kuiba umeme uonane na wanayo husika na wakupe utaratibu wa kuitumia umeme,
- ❖ Wakati unatembea na zafa uwe na udhu ili wakati wa swala ikiingia uweze kuswali na jamaa, wapenzi wa mtume hawawezi kuacha swala pamoja na jamaa.
- ❖ Katika zafa usiwalete farasi na ngamia kwani wanaweza kuwachafulia nguo waislamu kwa mkojo au kinyesi.
- ❖ Katika zafa uwagawie vitabu au risala iliyochapwa na Maktaba-tul-Madina na ikiwezekana uwape vcds za bayaan na kadhalika pia unaweza kuwapa matunda na vinywaji. Zingatia usiwatupie bali uwape mikononi mwao kwani inaweza ikaanguka chini ardhini na watu wakaikanyaga na itakuwa nje ya nidhamu.
- ❖ Uzingatie usilumbane na watu unaweza kuharibu nidhamu ya zafa kwa kukaa kimya ni manufaa yetu.

- ❖ Mwenyezi Mungu atuepushe hata kama mmerushiwa mawe msiwajibu kwa kuwarushia bali mvumilie kwani utakuja kuvuruga zafa yako na mpinzani akafurahi.

*Ghunchay chaikhay phūl mahkay har taraf āyī bahār*

*Ĥo gayī Ṣubḥ-e-Bahārān Eid-e-Milād-un-Nabī*

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

## Barua ya Attar inayo husiana na uzawa wa Mtume

(Ni ombi ya kimadani Ifikapo wiki ya mwisho wa mwezi wa Saffarul Muzaffar kila mwaka na kilapahali mkumbuke kusoma barua yangu na kuwa kumbushia akina Baba na akina Mama katika ijtimai zao.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Ni ombi ya Kimadani Kwa niaba ya Shekhe Tariqat Amir Ahle-Sunnat Maulana Muhammad Ilyas Attar Qadri Razwi Ziyaii دَامَتْ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَةَ Anatoa salamu kwa wapenzi wa mtume akina Baba na akina Mama.

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ  
الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ عَلَى كُلِّ حَالٍ

*Tum bhī kar kay un kā charchā apnay dil chamkō  
Aūnchay mayn aūnchā Nabī kā jhāndā ghār ghār mayn lahrō*

- ❖ Baada ya kuona mwezi umeandama basi watangazie waislamu Msikitini mara tatu. Na kisha wapongeze akina baba na akina Mama yakuwa mwezi ume andama wa Rabiul- Noor Shariff.

*Rabī'-un-Nūr ummīdaun kī dunyā sāth lay āyā  
Du'āon kī qabūliyyat ko hāthāun hāth lay āyā*

- ❖ Kwa akina Baba wanaopunguza ndevu zao na kuondoa kabisa ni haram kwao. Pia akina Mama wasio vaa baibui na hijabu ni haramu. Kwa Baraka ya mwezi mtukufu wa Rabiul Noor Shariff Kwa wale waislam wasio pamba ndevu basi wanuie kuwa wata pamba ndevu isiyo pungua kiganja cha mkono kwa siku zote za uhai wake na akina Mama pia wanuie kuwa watavaa baibui yaki Madani pamoja na hijabu siku zote za uhai wao. (Na wale akina Baba waliopunguza ndevu zao na kukata na akina Mama kukaa bila hijabu basi watubu kwani ni wajibu juu yao.)

*Jhuk gayā Ka'bah sabhī but munh kay bal aundhay giray  
أَهْلًا وَسَهْلًا مَرْحَبًا، دَاب-دَابْ أَحْمَد كَا ثَا،*

- ❖ Kwa kupata Istiqama kwa wapenzi wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akina Baba na akina Mama kila siku wajaze Madani

Inama'at na kumkabidhi Nigraan kila mwisho wa mwezi  
إِنْ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ .

*Badliyān raḥmat kī chāen būndiyān raḥmat kī āen*  
*Ab murādayn dil kī pāen āmad-e-Shāḥ-e-Arab ḥay*

- ❖ Wapenzi wote wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ hasa (amir) yaani nigraan na wale walio na madaraka waweke nia ya kusafiri ndani ya mwezi mtukufu wa Rabi-ul-Noor Shariff kwenye Madani qafilah ya siku tatu na akina Mama mwezi huu muwe mna toa mawaidha majumbani mwenu kwa wanawake wenzenu kwa siku 30 kwa kutumia kitabu cha Faizan-e-Sunnah Nakisha uweke azma yakutoa darsa siku za kawaida pia.

*Lūīnay raḥmatayn Qāfilay mayn chalo*  
*Sīkḥnay Sunnatayn Qāfilay mayn chalo*

*Kupata Rehma Twende kwenye Qafila ,*  
*Kufunza Sunnah, Twende Kwenye Qafila*

- ❖ Msikitini, madukani, viwandani, majumbani N.k mpambe kwa bendera 12 kama ikiwezekana la hata moja usikose kwa ajili ya mwezi mzima wa RABI-UL-NOOR SHARIFF. Wenye vyombo vya usafiri kama malori, mabasi, matrella, taxi, bajaji pikipiki N.K wanunue bendera na kuzifunga, إِنْ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ Kila sehemu itaonekana bendera za kijani



kibichi zina pepea na kuleta furaha.Ukizingatia kwenye malori, mabasi, utaona picha za ajabu zimebandikwa au kuandikwa maneno ya ajabu. Nawashauri wapenzi waislamu katika vyombo vyenu vya usafiri muandike maneno ya fuatayo,mimi nina mapenzi na Dawat-e-Islami kabla ya kuandika ushauriane na muhusika wa chombo hicho.

## Tahadhari

Kama kwenye bendera imechorwa kiatu tukufu cha Mtume wetu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Au imeandikwa aya yeyote basi uzingatie isiwe ina pepea na kuanguka chini itakuwa nje ya nidhamu,na pindi utapomalizika mwezi mtukufu wa Rabi-ul-Noor Shariff basi msichelewe kuteremsha bendera haraka kama huwezi kuzingatia basi uweke isiyo na mandishi yeyote wala picha yeyote.

Shekhe wetu mwenyewe anaweka nyumbani kwake bendera zisizo chorwa wala kuandikwa mandishi yeyote.

*Nabī kā jhāndā lay ker niklo duniyā mayn chā jāo*

*Nabī kā jhāndā aman kā jhāndā ghār ghār mayn lahrāo*

- ❖ Wapenzi waislamu majumbani mwenu mpambe kwa taa za kumulika mulika na kama ukikosa basi upambe kwa balbu 12 kwa ajili ya mwezi wa Rabi-ul-Noor Shariff kuanzia tarehe mosi hadi tarehe 12 lakini uonane na watu

wa shirika la umeme wakuruhusu kutumia umeme kwenye eneo lako na upambe na unga'rishe kwa balbu za rangirangi kama anavyopambwa biharusi. Dari za Miskiti, majumba na viwanja kwa kuzingatia waendesha magari, pikipiki na watembea kwa miguu kwa kuzingatia Huququl Amma na uninginize bendera yenye mita 12, usichimbe barabara na kuweka nguzo na kufunga bendera. Pia usichimbe mitaani inaweza ikabana njia kwa wale wanao pita na kusikitika kwa ajili ya njia finyu.

*Aik mashriq, aik maghrib, aik bām-e-Ka'bah per*

*أَهْلًا وَ سَهْلًا مَرْحَبًا، Naṣb parcham ḥo gayā,*

- ❖ Muislamu mwenye uwezo anunue vitabu, risala na majarida kutoka Maktaba-tul-Madina na agawe kwenye zafa na akina Mama pia wagawe. Hivyo hivyo kama tukiweka adhima ya kuweka vitabu madukani mwetu na tuwagawie watu ndani ya mwaka moja italeta mabadiliko. Mnaweza pia kunuia kwa ajili ya marehemu wetu na kuwapelekea thawabu, na uwaelimishe waislamu kufanya hivyo hata kwenye shuguli za harusi mnaweza kuwagawia risala na uchume thawabu.

*Bāni kar Madanī rasāil Dīn ko pḥaylāīye*

*Kar kay rāzī Ḥaq ko ḥaqdār-e-jinā ban jāīye*

- ❖ Amire Ahle Sunnat ameandaa kiperushi kilicho kuwa na maua 12 ya Kimadani kwa ajili ya uzawa wa Mtume na ikiwezekana kila mwislamu anunue risala 112 kutoka Maktaba-tul-Madina na kama huwezi basi japo risala 12 na kuzigawa na ujaribu kuwafikishia wakubwa wa Taasisi zinazoandaa Uzawa wa Mtume. Ndani ya mwezi wa Rabi-ul-Noor Sharif ikiwezekana mpatie Shekhe wa kisuni shilling elfu 12 na kama haiwezekani basi mpe shilligi 1200 na hata hii ikishindikana basi mpe shilling 12, au unaweza hata kupeleka Msikitini kwako na ukawagawia Imam, Muazini au Waangalizi wa Msikiti na ni bora zaidi kama ukinuia utatoa kila mwezi, ni fadhila zaidi ukitoa siku ya ijumaa kwani utapata faida mara ( 70 )

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ Baada ya kusikia kanda za Mawaidha za Sunna kuna habari ya kuwa watu wengi wamejirekebisha hata watakuwepo baadhi ya watu kati yenu baada ya kusikia kanda hii watakuwa wamejumuika na mazingira ya Dawat-e-Islami. Watu wengi wamefuata Sunna za Mtume kwa hiyo hata vcds hizo mnunue na kuwagawia waislamu ni jambo moja kubwa sana na utapata thawabu .Yule mwenye uwezo basi anunue vcd au audio kwa wiki mara moja au kwa mwezi mara moja na kuuza. Matajiri wanunue na wawagawie waislamu bure, na ikiwezekana ununue risala na ukaambatanisha na kadi ya mualiko wa harusi. Pia unaweza kugawa risala za dini badala ya

kufanya gharama ya kununua kadi za Iddi na kuwagawia waislamu utapata thawabu .

Sheikhe wetu Amir-Ahle Sunnat, Anasema waislamu wengi wananitumia kadi nzuri za Iddi kwa ajili ya kunipongeza zenye gharama kubwa ili niweze kufurahi lakini roho yangu inakasirika sana laiti pesa zao wangetumia kwa ajili ya dini basi inge kuwa bora zaidi.

*Un kay dar pay palnay wālā apnā āp jawāb*

*Koī Gharīb Nawāz to koī Dātā lagtā hāy*

- ❖ Katika miji mikubwa kila Nigraan (Amiri) aadhimishe Uzawa wa Mtume kwa muda wa siku 12 kwenye Misikiti tofauti tofauti, na akina mama washerekee uzawa wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ majumbani mwao kwa siku (12). Akina baba ikiwezekana kila mtakapo jumuiika kusherekea Uzawa wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ basi muende na bendera zenu ili muweze kupeperusha katika mahafali.

*Lab par Na'at-e-Rasūl-e-Akram hāthāun mayn parcham*

*Dīwānah Sarkār kā kitnā piyārā lagtā hāy*

- ❖ Ifikapo tarehe 11 ya Rabi-ul Noor Sheriff wakati wa usiku au siku ya tarehe 12 uoge asubuhi ikiwezekana unuie kwa ajili ya taadhima ya siku hiyo na uvae kanzu nyeupe, kilemba cha kijani na uweke tishadi ya rangi nyeupe juu ya

kilemba na uweke tishadi ya rangi ya kahawia kwa ajili ya kustiri pia ununue kitana, mafuta ya nywele, uturi viatu, kalamu, daftari, mswaki na saa kwa ajili ya matumizi yako. (Na Akina Mama Ikiwezekana Vitu Vya Mahitaji Yake Anunue Vipya).

*Āyī nayī ḥukūmat sikkāḥ nayā chalay gā*  
*‘Ālam nay rang badlā subḥ-e-shab-e-wilādat*

- ❖ Tarehe 12 ya Rabi-ul Noor Shariff waislamu mkeshe Msikitini hadi itakapo fika alfajiri na kabla ya kufika alfajiri mchukue bendera na kumswalia Mtume *صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ* kwa unyenyekevu kutoa machozi na kuukaribisha muda wa Uzawa wa Mtume *صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ* na baada ya hapo uswali swala ya alfajiri na uonane na waislamu wenzako na kuwapa mikono ya Iddi na kuwapongeza.

*Eid-e-Mīlād-un-Nabī to Eid kī bhī Eid ḥay*  
*Bil-yaqīn ḥay Eid-e-Eidān Eid-e-Mīlād-un-Nabī*

- ❖ Mtume wetu *صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ* alikuwa akifunga swamu siku ya jumatatu tatu kwa ajili ya kufurahia kuzaliwa kwake na ninyi pia mfunge siku ya tarehe 12 kwa ajili ya furaha ya Uzawa wa Mtume wetu *صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ* na mjumuike kwenye zafa huku mkiwa mmeinua bendera. Ikiwezekana mkae na udhu huku mkimswalia Mtume *صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ* na mkisoma Qasida kwa kutembea,

kutembea mwendo mzuri sio kutembea kwa kurukaruka na ukawapa watu nafasi ya kuzungumza nakukusema.

*Rabī'-ul-Awwal Aḥl-e-Sunnat tujḥ par kyūn na ḥaun qurbān*  
*Kay tayrī Bārḥwīn tārīkh woh Jān-e-Qamar āyā*

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

## Nia ya kusherekea maulidi

Katika kitabu cha Bukhari hadithi ya kwanza kabisa kuhusiana na nia **إِنَّمَا الْأَعْمَالُ بِالنِّيَّاتِ**. Kumbuka kuwa kila amali njema unuie kwajili ya akhera lasivyo hutapata thawabu.

*(Ṣaḥīḥ Bukhārī, Vol. 1, pp. 5)*

Hata ukisherekea Uzawa wa Mtume **صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ** lazima unuie na upate thawabu kwa ajili ya amali njema lakini kwa kufuata masharti zake. Kama mtu anasherekea au anaandaa kwa ajili ya kupata umaarufu na kwa ajili yake akaiba umeme ama akalazimisha watu kutoa michango na bila ruhusa ya wahusika na ukawasumbua wagonjwa, watoto wanao nyonya, watu walio pumzika na ukaweka paza sauti bila kuzingatia Huququl Amma basi badala ya kupata thawabu utapata dhambi. Kila nia ikiwa nyingi na nzuri basi thawabu pia zitakuwa nyingi. Nia 18 tunaziandika na sio mwisho, Wenye elimu wana weza kuongezea nia nzuri kwa ajili ya kuongeza thawabu.

## Kwa niaba ya herufi 18 za marhaba uzawa wa Mtume na nia 18 za kusherekea

- ❖ Nitasifu neema kubwa ya Allah **عَزَّوَجَلَّ**.

**وَأَمَّا بِعِصْمَةِ رَبِّكَ فَحَدِّثْ** 

- ❖ Kwa kupata ridhaa ya Allah **عَزَّوَجَلَّ** nitapamba taa, bendera na kusherekea Uzawa wa Mtume **صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ**.
- ❖ Sayyidunā Jibrāīl **عَلَيْهِ السَّلَام** aliweka bendera tatu wakati waku zaliwa kwa Bwana Mtume **صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ** na mimi nita zipeperusha bendera.
- ❖ Kwa kufananisha Quba ya kijani mimi nita peperusha bendera za kijani.
- ❖ Nita andaa kwa ukamilifu kabisa ili makafiri wajue Utukufu wa Mtume **صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ** kwa hakika wakiona nyumba hadi nyumba kuna taa zinamulika na bendera zina pepea watajua waislamu jinsi gani wanavyo mpenda Mtume wao **صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ**.

- ❖ Nitasherekea Uzawa wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kwa shangwe kabisa ili shetani ahuzunike.
- ❖ Vile nitavyo pamba kwa mapambo dhahiri na nita tubu na kuleta istighfar na nitajirekebisha undani wangu pia.
- ❖ Tarehe 12 kwenye ijtima na qasida.
- ❖ Nitasherekea Uzawa wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na nitashiriki kwenye zafa na kumzukuru na kumtakia rehema Mtume wetu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ.
- ❖ Nita wazuru Ulamaa.
- ❖ Watu wema.
- ❖ Wapenzi wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na kupata Baraka.
- ❖ Katika zafa nita kuwa nimevaa kilemba.
- ❖ Nitakuwa na udhu kipindi chote.
- ❖ Wakati nikiwa kwenye zafa nita zingatia nyakati za swala kusali kwa jamaa.



- ❖ Nikiwa na uwezo nitanunua vitabu kutoka maktaba tul-Madina, risala na kanda za bayaani zenye Sunna nakuwagawia waislamu kwenye zafa na Maulidi.
- ❖ Nitajaribu kuwaalika watu 12 kwa ajili ya safari ya Madini Qafilah.
- ❖ Wakati wa kutembea kwenye zafa nitajaribu kuweka kufle Madina ya ulimi na macho na kusikia qasida kwa umakini na kumswalia Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kwa wingi.

Yaa Ilahii utujaliye nyoyo zetu zifurahi na tuweze kufanya nia nzuri na utujaliye tuadhimishe Uzawa wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na kwaniaba yake utujaliye nafasi kwenye pepo ya Jannatul-Firdoz.

*Bakhsh day hām ko Ilāhī! Bahr-e-Milād-un-Nabī  
Nāmah-e-a'māl 'iṣyān say mayrā bhārpūr hāy*

*(Wasāil-e-Bakhshish, pp. 477)*

أَمِينٌ بِجَاهِ النَّبِيِّ الْأَمِينِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

## Baraka Za Sunnah

Katika mazingira mazuri ya Dawat-e-Islami (Shirika la Kimataifa la Kueneza Mafundisho ya Quran na Sunna lisilolijuhisha na siasa) sunna za Bwana Mtume **حَلِّ اللّٰهِ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّمَ** zinafunzwa kwa wingi.

Ni ombi kwa kila muislamu kuhudhuria na kukesha usiku mzima kwa nia ya kutaka radhi za Allah **رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ** pamoja na niya zingine nzuri katika ijtimai ya kila wiki siku ya Alhamisi baada ya sala ya Magharibi inayofanyika katika mji anaoishi. Vile vile ni ombi kwa kila muislamu kusafiri na wapenzi wa Mtume **حَلِّ اللّٰهِ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّمَ** katika Madani Qafila kwa nia ya kupata thawabu na kujifunza sunna za Bwana Mtume **حَلِّ اللّٰهِ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّمَ**. Na afanye Fikr-e-Madina (kujisaili mwenyewe) kwa kujaza kadi ya Madani In'amaat na amkabidhi Zimmedaar (msimamizi) wake katika siku kumi za mwanzo za kila mwezi. Kwa Baraka ya kufanya hivyo **بِنِهَا اللّٰهُ عَزَّوَجَلَّ** tutaweza kushikamana na sunnah za Mtume **حَلِّ اللّٰهِ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّمَ** na tutachukia maasi na tutazidi kuwa na hamu ya kulinda imani yetu.

Kila muislamu aweke azma ya kwamba: "Nitajaribu kusuluhisha nafsi yangu na watu wote wa ulimwengu mzima" **بِنِهَا اللّٰهُ عَزَّوَجَلَّ**

Kwa ajili ya kusuluhisha nafsi yangu nita fuata Madani In'amaat na kusuluhisha nafsi za watu wa ulimwengu nita safiri katika Madani Qafilah. **بِنِهَا اللّٰهُ عَزَّوَجَلَّ**



ISBN 978-969-579-343-5



0109479

Aalami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah, Mahallah Saudagaran  
Purani Sabzi Mandi, Bab-ul-Madinah, Karachi, Pakistan.

UAN: +92 21 111 25 26 92 | Ext: 1262

Web: [www.dawateislami.net](http://www.dawateislami.net) | E-mail: [translation@dawateislami.net](mailto:translation@dawateislami.net)